

Uteuzi wa Lugha katika Mahubiri ya Kikristo Jijini Nairobi

Alex Umbima Kevogo¹ na Mosol Kandagor²

¹*Chuo Kikuu cha Garissa*

²*Chuo Kikuu cha Moi*

Ikisiri

Makala haya yalichunguza hoja zilizoathiri uteuzi wa lugha iliyotumiwa na wahubiri wa Kikristo jijini Nairobi katika mahubiri yao. Wahubiri kadha kutoka kwa makanisa mbalimbali walishirikishwa katika utafiti huu. Wahubiri hao walihitajika kujaza hojaji na vilevile kushiriki kwenye mahojiano ya ana kwa ana wakati wa kukusanya data. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa hoja zilizoathiri uteuzi wa lugha katika mahubiri ya Kikristo jijini Nairobi ni pamoja na: aina ya washiriki katika mazungumzo, muktadha wa mazungumzo, yaliyomo kwenye mazungumzo, uamilifu wa mazungumzo na malengo ya mazungumzo. Aidha, tuligundua kuwa wahubiri wa Kikristo jijini Nairobi waliteua lugha ya kutumia katika mahubiri wakizingatia jukumu mahususi ambalo lingetekelezwa na lugha iliyoteuliwa kufanikisha malengo yao ya Kimawasiliano. Utafiti unabainisha umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika kufanikisha mawasiliano ya kidini katika maeneo yaliyo na sifa ya wingilugha.

Maneno Muhimu: Mahubiri, Muktadha, Wingilugha, Lugha

Utangulizi

Umuhimu wa Kiswahili katika kueneza na kutangaza dini katika eneo la Afrika Mashariki ulidhihirika vizuri mnamo karne ya kumi na tisa. Mashirika mengi ya kimishenari yalitambua kuwa kutokana na hali ya wingilugha, lugha ya Kiswahili ndiyo ambayo ingeweza kutumiwa kuhubiri na kueneza Injili ya Kristo kwa mafanikio makubwa (Chimerah, 1998). Kwa hiyo, Kiswahili kilitumiwa, kinatumiwa na kuna matumaini makubwa kwamba kitaendelea kutumiwa katika kutangaza na kuhubiri dini ya Kikristo.

Uteuzi wa lugha ni hali ya kuchagua kwa uangalifu neno, kishazi, kirai au sentensi ya lugha moja miongoni mwa zile lugha anazozijua mzungumzaji (Dweik na Qawar, 2015). Wanawingilugha na wanaujozilugha huchagua lugha moja dhidi ya lugha nyingine bila kupanga au kuratibu uamuzi wanaoufanya. Hii ina maana kuwa wazungumzaji wa lugha mbili au zaidi wanapotangamana, hulazimika kuteua lugha watakayoitumia katika mazungumzo yao. Kimsingi ni kwamba, wazungumzaji hao huteua sajili, mtindo, msimbo au toni ya sauti kwa kutegemea yule wanayewasiliana naye, mada ya mazungumzo yao, muktadha wa mazungumzo na njia ya mawasiliano wanayoitumia (Fasold, 1990).

Kuna sababu mbalimbali zinazochangia uteuzi wa lugha. Kwa mujibu wa Maya (2006) uteuzi wa lugha unaofanywa na mzungumzaji huathiriwa na sababu anuwai zikiwemo hadhi ya mzungumzaji katika jamii, jinsia, kiwango cha elimu, umri, mada ya mazungumzo, mahali pa mazungumzo, chimbuko la mzungumzaji, urasimi wa mazungumzo na msimbo unaotumiwa. Kwenye utafiti huu, wasailiwa waliulizwa kutaja sababu za kupenda kutumia lugha moja dhidi ya nyingine katika mahubiri ya Kikristo jijini Nairobi.

Matukio muhimu ya ibada ya Kikristo yanaweza kugawanywa katika sehemu maalumu. Sehemu hizo ni zile zinazohusu liturujia, kusifu na kuabudu, usomaji Biblia, mahubiri, maombi na toba na sadaka (Omoniyi 2012; Kouega 2008). Uchanganuzi wa matukio ya kidini kimgao unaweza kutumiwa kuonyesha uhusiano uliopo baina ya matumizi ya lugha na matukio ya kidini. Kupitia kwa utaratibu huu, sehemu bainifu za ibada hutengwa na kuchunguzwa ili kubainisha jinsi lugha inavyotumika kutimiza malengo mahususi ya kidini yanayokusudiwa. Uamuzi kuhusu lugha itakayotumika katika sehemu mahususi ya ibada huongozwa na maswali yafuatayo: ni lugha ipi inayoeleweka vyema na waumini wengi kwenye ibada? Ni lugha ipi inayozingatia sera ya kanisa? Ni lugha gani inayoendeleza vyema itikadi ya kidini ya kanisa husika? Ni lugha zipi zinazozungumzwa na mhubiri na kwa makusudi yapi? Mbali na kujibu baadhi ya maswali haya, utafiti huu ulichunguza sababu za kuteua lugha ya kutumiwa katika mahubiri ya Kikristo jijini Nairobi.

Kimsingi utafiti huu ulichunguza sababu za kimawasiliano zinazochangia uteuzi wa lugha unaofanywa na wahubiri wa Kikristo wanapochagua lugha ya kutumia katika mahubiri jijini Nairobi. Utafiti huu ulijaribu kubainisha kwamba popote ambapo mtu huhitajika kuteua kitu kimoja miongoni mwa vingine husaidiwa katika uteuzi huo na sababu fulani au imani aliyonayo kuhusu kufaa au kutofaa kwa kitu hicho anachokichagua. Imani au sababu hizo hutokana na tajiriba aliyopata mtu huyo na hukuza mielekeo yake. Mielekeo kama matokeo ya fikra huathiri vitendo vya mtu. Kutokana na hali kuwa Jiji la Nairobi ni jamii lugha ya wingilugha, wahusika huhitajika kuteua na kutumia lugha moja badala ya nyingine. Katiba ya Kenya inatambua Kiswahili na Kiingereza kama lugha rasmi. Lugha hizi ndizo hutumiwa nchini katika mahubiri. Iitarajiwa kuwa Wakenya wangukuwa na mielekeo chanya kuhusu matumizi ya lugha hizo ili kufanikisha sera ya kikatiba kuhusu lugha nchini. Kwa hivyo, lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza jinsi hoja za kimsingi zilizoathiri uteuzi wa lugha iliyotumiwa na wahubiri katika mahubiri ya Kikristo jijini Nairobi.

Utafiti wa Blom na Gumperz (1972) ulichunguza uteuzi wa lugha na ubadilishaji msimbo katika kijiji cha Hemnes huko Norway. Matokeo ya utafiti wao yalibainisha kuwa uteuzi wa lugha hutawaliwa na mfumo wa kijamii na kiuchumi wa watumizi wa lugha hizo. Ingawa utafiti huo ulitoa mwelekeo mkuu kwa upande wa njia za utafiti, ni bayana kuwa ulishughulikia suala la ubadilishaji msimbo tu.

Uchunguzi huu wa sasa uliofanyika jijini Nairobi ulichunguza uteuzi wa lugha katika muktadha wa mahubiri ya Kikristo.

Parkin (1974) alitafiti kuhusu ubadilishaji msimbo katika soko la Kaloleni jijini Nairobi. Wasailiwa katika utafiti wake walikuwa wafanyabiashara na wateja wao katika soko hilo. Ijapokuwa uchunguzi wake unatubainishia matokeo muhimu kuhusu matumizi ya lugha jijini Nairobi, lugha zilizotumika ni Kiswahili, Kikuyu, Kiluhya na Kijaluo. Matokeo ya utafiti huo yalionyesha kuwa lugha iliyotumiwa katika mazungumzo mengi ya kibiashara baina ya wauzaji na wanunuzi ilikuwa Kiswahili. Hata hivyo, baadhi ya wafanyabiashara walibadili msimbo na kuzungumza lugha za asili pindi walipogundua kuwa wateja wao walizungumza lugha hizo. Huu ubadilishaji msimbo ulilenga kuwashawishi wateja kwa urahisi ili wanunue bidhaa zilizokuwa zinazuzwa. Utafiti huo ulikuwa muhimu kwa utafiti huu wa sasa kwa sababu uliangazia hali ya matumizi ya lugha ya jiji la Nairobi ambalo ndilo lililokuwa eneo la utafiti huu. Hali hiyo, hata hivyo, ilitofautiana na ile iliyochunguzwa kwenye utafiti huu kwa vile ulitumia muktadha tofauti wa kanisani. Vilevile utafiti wa sasa ulihusisha eneo pana kijiografia lililo la jiji la Nairobi.

Katika utafiti uliofanyika eneo la Oberwart nchini Austria, Gal (1979) aligundua kuwa kuna uhusiano kati ya uteuzi wa lugha inayotumiwa katika mazungumzo na hali ya kijamii na kiuchumi ya wazungumzaji lugha husika. Utafiti huo ulifanyika katika jamii iliyo na sifa ya wingilugha japo wakazi wake walikuwa na uwezo tofauti wa kiuchumi. Lengo la utafiti huo lilikuwa kuchunguza mielekeo ya wanajamii kuhusu lugha ya Kijerumani na Kihangari. Mielekeo ya wanajamii kuhusu lugha ilitumiwa kueleza sababu za uteuzi wa lugha moja dhidi ya nyingine. Kwa upande wake, utafiti huu wa sasa ulifanyika katika jiji la Nairobi ambalo pia lina hali ya wingilugha. Hali hii ilitupa msukumo kutaka kuhusisha matumizi ya lugha katika mahubiri ya Kikristo na hali halisi ya kijamii na kiuchumi jijini Nairobi. Fauka ya hayo, utafiti huu ulichunguza iwapo kuna hoja zinazoathiri uteuzi wa lugha wanayoitumia kuhubiri katika ibada.

Myers-Scotton (1980) alichunguza uteuzi wa lugha katika jamii za mijini nchini Kenya zinazozungumza lugha nyingi. Matokeo ya utafiti wake yanathibitisha kuwa uteuzi wa lugha unaweza kuhusishwa na sifa za kijamii za wazungumzaji na pia hali na mahali wanapojipata. Matokeo ya utafiti huo yalionyesha kuwa uteuzi wa lugha fulani unaweza kueleweka katika muktadha maalumu wa maingiliano ambamo uteuzi huo hutokea. Hii inamaanisha kwamba ni ule muktadha aliomo mtu unaomfanya ateue lugha fulani inayostahiki kufanikisha mawasiliano. Mawazo hayo yalikuwa muhimu kwa utafiti huu wa sasa kwa vile ulitafiti sababu za uteuzi wa lugha unaofanywa na wahubiri wa Kikristo jijini Nairobi. Uchunguzi huu ulilenga kuthibitisha iwapo kuna hoja zinazoathiri uteuzi wa lugha inayotumiwa katika mahubiri ya Kikristo jijini Nairobi yanayofanyika katika muktadha wa wingilugha.

Uteuzi wa lugha unaweza kutumiwa kuonyesha umuhimu wa mwelekeo wa mazungumzo lakini athari za mawasiliano za lugha maalumu iliyoteuliwa

hutawaliwa na kaida za kijamii (Kendal, 1980). Mawazo haya yalikuwa na umuhimu katika utafiti huu wa sasa kwa sababu mojawapo ya malengo yake lilikuwa kuchunguza hoja zinazochangia uteuzi wa lugha ya kutumia katika mahubiri jijini Nairobi. Hili lilifanikishwa kupitia uchunguzi kuhusu kaida za kijamii zinazotawala mawasiliano katika muktadha wa mahubiri ya Kikristo.

Uchunguzi wa Platt (1980) kuhusu uteuzi wa lugha ulionyesha kuwa katika jamii yenye lugha nyingi zilizo na hadhi tofautitofauti, uteuzi wa mojawapo ya lugha hizo hautegemei kama mzungumzaji wa lugha hizo anajua lugha ngapi tu bali pia hutegemea lugha anazozijua yule anayepokea ujumbe. Kwa upande wake, utafiti huu ulifanyika katika jiji la Nairobi ambalo lina hali ya wingilugha. Hii inamaana kuwa wakazi wa jiji la Nairobi wanaozungumza lugha nyingi hukabiliwa na uamuzi wa kuteua lugha watakayoitumia kufanikisha mawasiliano yao. Hali hii ilichunguzwa kwenye utafiti huu kwa kuzingatia mfano wa matumizi ya lugha katika mahubiri ya Kikristo.

Suala la uteuzi na matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi wa shule za msingi jijini Nairobi limefanyiwa utafiti na Wangia (1992). Lengo la utafiti huo lilikuwa kuchunguza viwango vinavyotofautiana vya matumizi ya Kiingereza, Kiswahili, Sheng' na lugha za asili miongoni mwa wanafunzi wa darasa la kwanza hadi la tatu. Wasailiwa waliteuliwa kutoka katika mitaa iliyo na wakazi wenye uwezo tofautitofauti wa kiuchumi. Madhumuni mahususi ya utafiti huo yalikuwa kuchunguza jinsi watoto wanavyotumia lugha za asili jijini Nairobi. Aidha, utafiti huo ulidhamiria kuchunguza majukumu yanayotekelezwa na Kiingereza na Kiswahili kama lugha za kwanza za baadhi ya watoto. Utafiti huo uliazimia pia kuchunguza sababu zinazopelekea uteuzi wa lugha unaofanywa na watoto jijini Nairobi. Matokeo ya utafiti huo yanaonyesha kuwa lugha za asili ndizo zinazotumika kwa nadra sana na watoto jijini Nairobi. Kiswahili ndiyo lugha ya mazungumzo katika mawanda mapana ya watoto wengi waliochunguzwa. Kwa upande mwingine, Kiingereza hutumiwa sana na watoto wanaotoka katika mitaa ya kifahari na iliyo na uwezo wa kiuchumi. Utafiti huo ulikuwa wa manufaa kwa utafiti huu wa sasa kwa sababu ulifanyika katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Nairobi ambayo yana wakazi wanaotofautiana kwa upande wa uwezo kiuchumi. Hata hivyo, utafiti huu ulijikita zaidi katika kuchunguza hoja zinazoathiri uteuzi wa lugha inayotumiwa katika mahubiri ya Kikristo.

Vijana wa kiume kutoka mitaa isiyo ya kifahari ya Eastlands wanapenda kutumia lugha ya Sheng' wakilinganishwa na wenzao katika mitaa ya kifahari ya Westlands (Fink, 2005). Utafiti huo uliofanyika katika mitaa ya Eastlands na Westlands ya jiji la Nairobi ulitumia hojaji kukusanya data. Wasailiwa waliainishwa katika makundi mawili kutegemea umri, tabaka na jinsia. Kundi la kwanza lilikuwa na umri wa baina ya miaka 18 na 29 na la pili miaka 30 na kuendelea. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa mielekeo ya vijana kuhusu lugha ya Kiingereza inabadilika kutoka hali ya kuipenda lugha ya Kiingereza hadi kuithamini na kuitumia Sheng'.

Vijana wa kike na watu wa tabaka la juu wanapenda kutumia Kiingereza. Watu wazima katika mitaa yote miwili wanapenda kutumia lugha za kabila ikilinganishwa na Kiingereza na Kiswahili. Wasailiwa wote walikubali kuwa lugha ya Kiswahili itumiwe na Rais anapolihutubia taifa. Utafiti wa Fink (2005) ulikuwa muhimu kwa mtafiti kwa sababu alizingatia Jiji la Nairobi na vilevile kuhusisha kigezo cha tabaka la wasailiwa. Utafiti huo pia unaangaza mielekeo ya wasailiwa wa umri na jinsia mbalimbali kuhusu Kiswahili, Kiingereza, Sheng' na lugha za kabila mbalimbali. Isitoshe, unaonyesha umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika nyanja ya utawala. Hata hivyo, utafiti huu wa sasa ulipiga hatua mbele na kuchunguza iwapo mielekeo ya wakazi wa jiji la Nairobi kuhusu lugha inaathiri jinsi wanavyoteua na kutumia lugha katika muktadha wa dini ya Kikristo.

Wingilugha ni mtaji unaosaidia uteuzi wa lugha kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali katika mawasiliano (Bamgbose, 1992). Hii ni kwa sababu lugha mbalimbali hutumiwa kutekeleza majukumu tofautitofauti kutegemea muktadha wa mawasiliano. Utafiti wa Ugot (2009) unachunguza hali ya uteuzi wa lugha kwa kuzingatia ubadilishaji msimbo na uchanganyaji msimbo katika muktadha wa wingilugha. Eneo la utafiti lilikuwa Biase nchini Nigeria. Utafiti huo uliazimia kuchunguza matumizi ya Kiingereza, Kiefiki, Kiigbo na Pijini ya Nigeria katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya kimawasiliano kwenye jamii ya Wabiase. Lengo la utafiti huo lilikuwa kuchunguza uteuzi unaofanywa na wazungumzaji wanapoamua kutumia lugha fulani kufanikisha mazungumzo kutegemea muktadha.

Matokeo ya utafiti huo yanaonyesha kuwa uteuzi wa lugha wa Wabiase huchochewa na sababu zifuatazo: elimu, dini, uchumi, shughuli za kijamii, utamaduni, utawala na matumizi ya lugha katika muktadha wa nyumbani. Utafiti wa Ugot (2009) unaonyesha kuwa Kiingereza ambayo ni lugha rasmi nchini Nigeria inatumiwa kufanikisha shughuli za utawala wa Biase. Isitoshe, lugha ya Kiingereza inatumiwa katika elimu, biashara na vyombo vya habari. Katika jamii ya Wabiase, Kiingereza kinatumika kufanikisha mawasiliano na wazungumzaji wengine wanaotoka katika jamii jirani na hata nje ya nchi. Hii ina maana kuwa Kiingereza ndiyo lugha ya hadhi ya juu inayopendelewa na asasi mbalimbali za kiserikali na zile za kijamii.

Kimsingi, Kiingereza ndiyo lugha ya utawala, elimu, biashara na mawasiliano ya kimataifa katika eneo la Biase. Kwa upande mwingine, Kiefiki ndiyo lugha inayoenea kwa kasi katika eneo la Biase kiasi cha kutumiwa kama lingua franka. Mbali na kuwa lugha ya biashara kuanzia karne ya kumi na nane, Kiefiki ndiyo lugha ya dini iliyofanikisha kuenea kwa dini ya Kikristo katika eneo la Biase. Hata hivyo, hivi karibuni Kiefiki kinakabiliwa na ushindani mkubwa kutoka kwa Pijini ya Nigeria. Kwa mujibu wa Ugot (2009) Kiigbo, ambayo ni lugha ya tatu iliyo na wazungumzaji wengi nchini Nigeria, kinazungumzwa katika eneo la mpaka wa Wabiase na Waigbo. Kiigbo kinatumiwa na baadhi ya Wabiase kama lugha ya shughuli za kitamaduni kwa mfano ndoa. Kwa hivyo, Kiigbo kimefanikisha ukopaji

wa baadhi ya tamaduni za Waibo miongoni mwa Wabiase. Pijini ya Nigeria inatumiwa katika shughuli zisizo rasmi za biashara na utawala.

Kwa upande mwingine, Pijini ya Nigeria ndiyo lugha ya utangamano wa kijamii. Matokeo ya utafiti huo yanaonyesha kuwa uteuzi wa lugha unategemea muktadha wa mazungumzo na shughuli inayotekelezwa. Hali hii imesababisha kuchanganya msimbo na kubadili msimbo ili kufanikisha mawasiliano. Wazungumzaji huchanganya au kubadili msimbo kutegemea muktadha, washiriki na mada ya mazungumzo. Kila mojawapo ya lugha zinazotumiwa katika eneo la Biase hutekeleza majukumu ya kijamii na kitamaduni. Utafiti wa Ugot (2009) ulikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa sababu ulitekelezwa katika eneo la wingilugha kama ilivyo jiji la Nairobi ambalo lina sifa ya wingilugha. Hata hivyo, utafiti huu ulilenga kuchunguza sababu za uteuzi wa lugha katika muktadha wa dini ya Kikristo.

Yakub, Matu na Ongarora (2012) walitafiti kuhusu matumizi na uteuzi wa lugha ya Kinubi katika nyanja ya nyumbani. Wasailiwa 30 wa jamii ya Wanubi wanaoishi katika mtaa wa Kibra jijini Nairobi walishirikishwa katika utafiti huo. Lengo kuu la utafiti huo lilikuwa kuchunguza jinsi Kinubi kinavyotumiwa katika nyanja ya nyumbani ili kufafanua sababu zinazowapelekea wazungumzaji wa Kinubi kuteua kukitumia. Data ilikusanywa kupitia kwa hojaji na utazamaji. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa wazungumzaji huhimiza matumizi ya Kinubi nyumbani kama njia ya kuhifadhi lugha yao. Uteuzi wa Kinubi dhidi ya lugha zingine huathiriwa na malengo ya wazungumzaji katika mawasiliano. Matokeo ya utafiti huo yanabainisha kuwa Kinubi ndiyo lugha inayopendelewa zaidi katika mazungumzo ya nyanja ya nyumbani. Utafiti huo ulikuwa na manufaa kwa utafiti huu kwa sababu ulifanyika pia jijini Nairobi. Lengo kuu la utafiti huu wa sasa lilikuwa kuchunguza hoja zinazoathiri uteuzi wa lugha inayotumiwa katika mahubiri ya Kikristo. Hii ina maana kuwa utafiti huu ulipiga hatua na kueleza wazi hoja zinazoathiri uteuzi wao wa lugha ya mahubiri ya Kikristo. Tafiti hizi zinatofautiana kwa sababu utafiti huu ulizingatia matumizi ya lugha katika muktadha wa dini.

Muktadha wa Kiisimujamii wa Eneo la Utafiti na Wasailiwa

Jiji la Nairobi ndilo jiji kuu la taifa la Kenya. Jiji la Nairobi ni miongoni mwa miji inayokua kwa kasi barani Afrika. Kwa mujibu wa ripoti ya sensa ya 2019, Jiji la Nairobi lina jumla la wakazi 4, 397, 073 (KNBS, 2020). Idadi kubwa ya wakazi wa jiji la Nairobi inatokana na uhamiaji mjini wa watu wanaotoka maeneo ya mashinani na hata miji mingine. Uhamiaji huo unatokana na sababu za kiuchumi, kijamii na hata kisiasa. Baadhi ya wahamiaji wanaotoka pande zote za taifa la Kenya huja jijini Nairobi kutafuta ajira na huduma bora za kijamii na kiuchumi. Jiji la Nairobi lina sifa ya wingilugha. Hali hiyo inatokana na kuwepo kwa wakazi wanaotoka katika jamii-lugha mbalimbali za taifa la Kenya. Isitoshe, kuna wakazi wanaotoka katika mataifa ya kigeni waliokuja kwa ajili ya ajira, biashara, ndoa au utalii. Baadhi ya lugha zinazozungumzwa na jamii za kigeni ni Kiingereza, Kifaransa, Kijerumani, Kihindi, Kijapani, Kichina na Kikorea.

Wakazi wengi wa Jiji la Nairobi wana umilisi wa lugha tatu. Kuna wakazi wanaozungumza lugha moja. Kwenye kundi hilo kuna wale wanaozungumza lugha zao za kwanza ambazo ni za kikabila. Wakazi wenye ujozilugha wanazungumza lugha zao za kikabila na lugha ya taifa yaani Kiswahili. Wakazi wenye sifa ya wingilugha wanazungumza lugha tatu. Lugha hizo ni zile za kikabila, lugha ya taifa na lugha ya kigeni ambayo ni Kiingereza. Baadhi ya wakazi huzungumza lugha nne au zaidi. Hali hii inaonyesha kuwa wakazi wa Jiji la Nairobi wanadhihirisha hali ya ujozilugha na wingilugha.

Utafiti huu ulishirikisha jumla ya wasailiwa 48 waliokuwa wahubiri wa Kikristo jijini Nairobi. Kati ya wasailiwa hao, wanawake walikuwa 20 ilhali wanaume walikuwa 28. Hii ina maana kuwa asilimia 42 ya wasailiwa walikuwa wanawake. Kwa upande mwingine, asilimia 58 ya wasailiwa walikuwa wanaume. Matokeo ya utafiti yalionyeshwa kuwa, wasailiwa walioshirikishwa kwenye utafiti huu walikuwa na umri wa kati ya miaka ishirini na mmoja na zaidi ya miaka arobaini

Utafiti huu ulitumia mbinu za utafiti wa nyanjani ili kubainisha hali halisi ya uteuzi na matumizi ya lugha katika mahubiri ya Kikristo yanayofanyika kanisani jijini Nairobi. Mbinu za utafiti wa maktabani zilitumiwa pia kwenye utafiti huu ili kumwezesha mtafiti kudhibiti mada ya utafiti kabla ya kufanya utafiti wa nyanjani. Utafiti ulifanyika katika maeneo bunge sita ya Jiji la Nairobi yaliyoteuliwa kimaksudi. Maeneo bunge hayo yalikuwa Lang'ata, Starehe, Dagoretti Kaskazini, Kibra, Mathare na Westlands. Uteuzi wa maeneo haya ulifanywa kimaksudi kutokana na sifa za kiuchumi na kijamii za wakazi wake na lugha zinazozungumzwa na wakazi wa mitaa ya maeneo haya. Kigezo cha uwezo wa kiuchumi na kijamii kilitusaidia kubainisha matabaka ya wakazi wa maeneo mbalimbali.

Katika eneo bunge la Westlands wadi za Kangemi na Parklands zilishirikishwa kwenye utafiti. Katika eneo bunge la Langata, wadi za Karen na Mugumoini zilihusishwa kwenye utafiti huu. Kwa upande wa eneo bunge la Starehe, wadi za Ngara na Ziwani zilihusishwa kwenye utafiti huu. Kwenye eneo bunge la Kibra, wadi za Woodley na Laini Saba zilishirikishwa katika utafiti huu. Aidha katika eneo bunge la Dagoretti Kaskazini wadi za Kileleshwa na Kawangware zilihusishwa kwenye utafiti huu. Isitoshe, kwenye eneo bunge la Mathare wadi za Huruma na Mlango Kubwa zilishirikishwa kwenye utafiti. Wadi hizi zilichaguliwa kupitia kwa uteuzi wa kudhamiria kwa sababu ya kuwa na wakazi wa tabaka la chini na lile la juu wanaotoka katika jamii lugha mbalimbali za Kenya. Kwa ajili ya kulinganisha na kulinganua jinsi lugha ilivyotumiwa katika muktadha wa dini katika mitaa ya kifahari, wastani na ile duni, ilitubidi tuhushishe wadi zilizotajwa.

Makanisa 48 yalishirikishwa katika utafiti huu. Makanisa manne yaliyotumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwenye ibada yaliteuliwa kinasibu kutoka kwa kila wadi iliyoshirikishwa kwenye utafiti. Wahubiri 48 kutoka kwa makanisa 48 walishirikishwa katika utafiti huu. Wahubiri hao walihitajika kujaza hojaji na vilevile kushiriki kwenye mahojiano ya ana kwa ana wakati wa kukusanya data.

Isitoshe, mtafiti alishiriki kwenye ibada za makanisa yaliyoshirikishwa kwenye utafiti na kurekodi mahubiri. Data ilichanganuliwa kwa kutoa maelezo kuhusu sababu za kuchagua lugha moja dhidi ya lugha nyingine ili kufanikisha mawasiliano.

Matokeo ya Utafiti

Data iliyokusanywa katika utafiti huu ilikuwa ya kithamano. Data ya kithamano ilikusanywa kupitia kwa mahojiano na hojaji. Kimsingi data hii ilihusu maelezo yaliyotolewa na wahubiri wenyewe. Hojaji na mahojiano yalitumiwa kukusanya data kuhusu lugha iliyotumiwa katika mahubiri ya Kikristo, sababu za kutumia lugha ya aina hiyo na umuhimu wa kutumia lugha hiyo katika mahubiri jijini Nairobi. Data hii ilichanganuliwa kwa mujibu wa maelezo ya kiisimu. Baadhi ya sababu zilizotolewa na wasailiwa ambazo ziliongoza uteuzi wao wa lugha moja dhidi ya nyingine katika mahubiri ya Kikristo jijini Nairobi zimejadiliwa katika sehemu inayofuata.

Kutumiza Malengo fulani ya Kimawasiliano

Wazungumzaji huteua lugha fulani dhidi ya lugha nyingine ili kukidhi mahitaji fulani ya kimawasiliano (Coulmas, 1997). Matokeo ya utafiti huu yanakubaliana na maoni hayo ya Coulmas (1997). Wahubiri wa Kikristo jijini Nairobi waliteua lugha ya Kiswahili katika mahubiri yao ili kutimiza malengo fulani ya kimawasiliano. Asilimia 25 (J=12) ya wasailiwa walieleza kuwa walipenda kutumia Kiswahili katika mahubiri yao kwa vile walijihisi kuwa karibu sana na hadhira yao. Hali hiyo inatokana na sababu kuwa waumini wao walitumia sana lugha ya Kiswahili katika mazungumzo yao ya kawaida. Kwa hiyo, wahubiri walitumia Kiswahili katika mahubiri ili kujenga uhusiano wa karibu na waumini wao. Asilimia 29 (J=14) ya wasailiwa walieleza kuwa hadhira yao ilikuwa na waumini waliokuwa na viwango vinavyotofautiana vya elimu. Kutokana na sababu hiyo, lugha ya Kiswahili ndiyo iliyofaa kuwasilisha ujumbe bila kuwatenga baadhi ya waumini. Asilimia 67 (J=32) ya wasailiwa walieleza kuwa wao huteua lugha itakayofanikisha uelewaji wa ujumbe unaohubiriwa kwa njia rahisi na kamilifu kwa waumini. Iwapo ujumbe huo utaeleweka vyema wanapotumia lugha ya Kiswahili kuliko Kiingereza, basi watalazimika kutumia lugha hiyo bila kuzuilwa na ratiba ya kutumia lugha fulani kwenye ibada.

Lugha ya Kiswahili, katika muktadha wa utandawazi unaowaleta pamoja wanajamii kutoka katika jamii mbalimbali ulimwenguni, imekuwa ni chombo muhimu cha mawasiliano. Wanajamii kutoka katika makabila mbalimbali hutangamana kidini wakitumia Kiswahili (Moshi, 2006). Hali hii imetokana na uwezo wa Kiswahili wa kutozingatia tofauti za kimbari na utambulisho wa kikabila. Wahubiri wa Kikristo jijini Nairobi wanaolenga kujenga utambulisho wa kitaifa usiopendelea kabila lolote hutumia lugha ya Kiswahili wanapohubiri kanisani. Kimsingi, tunaweza kuhitimisha kuwa, mielekeo chanya walio nayo wahubiri wa

Kikristo jijini Nairobi kuhusu lugha ya Kiswahili ndiyo inayowaongoza kuitumia ili kuafikia malengo mbalimbali ya kimawasiliano katika mahubiri.

Washiriki katika Mazungumzo

Washiriki katika mazungumzo ni dhana inayotumiwa kurejelea mzungumzaji pamoja na wapokezi wa ujumbe. Mzungumzaji katika muktadha fulani wa mazungumzo huwa na hiari ya kuchagua lugha, msimbo, mtindo, lahaja na hata launi atakayoitumia katika mawasiliano (Gumperz, 1964). Lengo la uchaguzi huo wa mzungumzaji huwa ni kutimiza malengo fulani ya kimawasiliano kwa njia iliyomwafaka zaidi. Gumperz (mtajwa) anaeleza kuwa uwezo wa mzungumzaji kuchagua msimbo, mtindo au launi inayofaa zaidi kukidhi malengo yake kimawasiliano kwa hadhira yake kwa ubora zaidi ni sehemu ya umilisi wake wa kimawasiliano. Mzungumzaji anapochagua lugha moja dhidi ya nyingine atakayoitumia katika mawasiliano huongozwa na aina ya hadhira anayowasiliana nayo. Aina ya hadhira au wapokezi wa ujumbe hutegemea umri, jinsia, hadhi, kiwango cha elimu na tabaka (Maya, 2006).

Asilimia 78 (J=38) ya wasailiwa walieleza kuwa uteuzi wao wa lugha ya kutumia katika mahubiri uliongozwa na aina ya hadhira ambayo walikuwa wanahubiria. Wasailiwa hao walifafanua kuwa walipokuwa wanaandaa mahubiri yao walijiuliza maswali fulani kuhusu wapokezi wao wa ujumbe. Baadhi ya maswali hayo ni: Ni watu wa tabaka lipi? Hadhi yao katika jamii ni ipi? Umri wao ni upi? Wengi ni vijana au watu wakomavu? Na idadi kubwa ya hadhira ina wastani wa kiwango gani cha elimu? Wasailiwa kwenye utafiti huu walieleza kuwa maswali hayo yaliwaongoza kuchagua sio tu aina ya ujumbe na njia ya kuuwasilisha bali pia lugha ya kutumia kuuwasilisha.

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti, ilibainika kuwa lugha zinazopendelewa zaidi katika mahubiri ya Kikristo yanayofanyika kanisani jijini Nairobi ni Kiswahili na Kiingereza. Wasailiwa wote walioshirikishwa kwenye utafiti huu walieleza kuwa ibada katika makanisa yao ziliendeshwa katika lugha ya Kiswahili na vilevile Kiingereza. Hata hivyo, kulikuwa na tofauti katika majibu ya wasailiwa walipoulizwa kutaja lugha walizopendelewa kutumia wakati wa kuhubiri kanisani. Asilimia 56 (J=27) ya wasailiwa walieleza kuwa walifurahia kuhubiri wakitumia lugha ya Kiswahili. Kwa upande mwingine, asilimia 44 (J=21) ya wasailiwa walieleza kuwa walipendelewa kutumia lugha ya Kiingereza wakati wa kuhubiri kanisani. Hii ina maana kuwa lugha inayopendelewa zaidi katika mahubiri ya Kikristo jijini Nairobi ni Kiswahili. Wasailiwa wote walikiri kuwa walilazimika kuchanganya lugha walipohubiri ili kufafanua hoja zao kwa waumini.

Kutokana na mielekeo chanya walio nayo wahubiri wa Kikristo jijini Nairobi kuhusu lugha ya Kiswahili, tunaweza kuhitimisha kuwa uteuzi wao wa lugha ya mahubiri uliathiriwa na mielekeo hiyo. Hili linatokana na wazo kuwa lugha ya Kiswahili hutumiwa kwa mafanikio makubwa kwa kila aina ya hadhira ya waumini

bila kujali tabaka lao, hadhi yao, kiwango chao cha elimu, umri wao, jinsia au muundo wa jamii yao kiuchumi na kijamii.

Muktadha wa Mazungumzo

Crystal na Davy (1969) wanaeleza kuwa muktadha ni yale mambo yanayozunguka eneo la matumizi ya lugha au mazungumzo. Kwa upande mwingine, Schiffirin (1994) anaeleza kuwa muktadha ni ulimwengu uliojaa watu wenye mahusiano tofauti, wenye mahitaji tofauti, wenye nia tofauti na wenye uwezo tofauti. Watu hawa wanaingiliana katika kufanya shughuli za kawaida za kila siku huku wakitawaliwa na kaida za utamaduni mahususi. Kaida hizo hutawala maingiliano yao ya kilugha. Ujumla huu wa watu na maingiliano yao ndio huunda muktadha. Kimsingi, muktadha hurejelea hali ambamo lugha hutenda kazi. Hali hizo zinaweza kuwa za kimazingira, kijamii au kiasasi ambazo hujumuisha matukio, wakati, utamaduni na kaida za kijamii zinazoathiri matumizi ya lugha. Muktadha wa mazungumzo uliohusishwa katika utafiti huu ulikuwa ule wa mahubiri ya Kikristo yaliyofanywa kanisani. Muktadha wa mahubiri ya Kikristo huwa na kaida na kanuni zake ambazo huathiri uteuzi na matumizi ya lugha.

Asilimia 86 (J=42) ya wasailiwa walieleza kuwa ratiba na sera za kanisa ziliathiri kwa kiasi kikubwa uchaguzi wa lugha iliyotumiwa katika mahubiri. Ibada kuu katika makanisa yaliyoshirikishwa kwenye utafiti ziliendeshwa katika Kiswahili au Kiingereza. Mhubiri alilazimika kutumia lugha iliyopendekezwa kwenye ibada husika. Wasailiwa walieleza kuwa iwapo mhubiri alikosa umilisi wa lugha iliyopendekezwa kwenye ibada, ilimbidi atumie lugha aliyomudu kisha ikakalimaniwa. Asilimia 56 (J=27) ya wasailiwa walieleza kuwa walifurahia kuhubiri wakitumia Kiswahili. Wasailiwa kwenye kundi hili walikuwa kutoka kwenye mitaa ya Huruma, Ziwani, Mugumoini, Mlango Kubwa, Laini Saba, Kangemi na Kawangware. Wasailiwa hao walieleza kuwa waumini kwenye makanisa yao walielewa vyema zaidi ujumbe uliohubiriwa katika lugha ya Kiswahili. Asilimia 44 (J=21) ya wasailiwa walieleza kuwa walifurahia kuhubiri wakitumia lugha ya Kiingereza. Wasailiwa kwenye kundi hili walikuwa wahubiri wa makanisa katika mitaa ya kifahari ya Karen, Kileleshwa, Parklands na Woodley.

Ibada kuu za makanisa kwenye mitaa ya kifahari ya Karen, Kileleshwa na Parklands huendeshwa katika Kiingereza. Ibada ya Kiswahili kwenye makanisa hayo hazikuwa maarufu. Asilimia 25 (J=12) ya wasailiwa katika mitaa ya Karen, Kileleshwa na Parklands walieleza kuwa ibada za Kiswahili katika makanisa yao zilikuwa na waumini wachache zikilinganishwa na zile za Kiingereza. Hali hii inaonyesha kuwa waumini huathiri lugha itakayotumiwa kwenye ibada. Kwenye mitaa isiyo ya kifahari wahubiri hutumia lugha ya Kiswahili inayoeleweka na waumini wengi kama chombo cha kujenga uhusiano wa karibu na utangamano na waumini wao. Lugha iliyotumiwa kwingi hapa ilikuwa ni lugha ya Kiswahili.

Yaliyomo kwenye Mazungumzo

Yaliyomo kwenye mazungumzo hujikita katika mada ya aina fulani kwa mfano dini, siasa, teknolojia, sayansi na uchumi. Mada ni kile kinachozungumziwa katika mawasiliano ya aina fulani (Hymes, 1964). Mahubiri yanayotendeka kanisani huangazia masuala ya kidini. Japo mahubiri ya Kikristo huangazia mada ya kidini kwa upana wake, ujumbe unaohubiriwa humulika vipengele mahususi vya dini ya Kikristo. Hii ina maana kuwa mahubiri yanaweza kuzingatia kipengele kimoja cha Ukristo kwa mfano ubatizo, imani, wokovu, toba na sala. Asilimia 69 (J=33) ya wasailiwa walieleza kuwa mada ya mahubiri iliathiri uteuzi wa lugha iliyotumiwa katika mahubiri ya Kikristo. Wasailiwa hao walifafanua kuwa kuna mada zilizo hitaji msamiati maalumu katika lugha moja ambao ingekuwa vigumu kupata visawe vyake katika lugha ya pili. Katika hali kama hiyo, wahubiri walilazimika kuchanganya lugha au kutoa maelezo ya ufafanuzi wa dhana husika katika lugha iliyoeleweka vyema kwa waumini.

Asilimia 54 (J=26) ya wasailiwa walieleza kwamba kuna ujumbe unaohusu mada fulani ambao ungehubiriwa kwa urahisi katika lugha fulani ikilinganishwa na lugha nyingine. Katika muktadha kama huo wasailiwa walilazimika kutumia lugha ambayo ingewasilisha ujumbe huo kwa waumini kwa urahisi. Kimsingi ni kwamba, mada ya mazungumzo, aina ya msamiati unaohitajika katika mazungumzo na ujumbe uliowasilishwa uliathiri uteuzi wa lugha iliyotumiwa katika mahubiri ya Kikristo jijini Nairobi.

Uamilifu wa Mazungumzo

Usemi unaotumiwa katika mawasiliano ya kidini hulenga kutimiza dhima fulani au vitendo maalumu vya kimawasiliano kwa mfano kuhimiza, kutawaza, kuonya, kukashifu au kupongeza (Austin, 1962 na Searle, 1969). Malengo haya yanaweza kutimizwa tu iwapo mzungumzaji na mpokezi wa ujumbe watawasiliana wakitumia msimbo unaoeleweka vyema kwao wote. Katika muktadha wa mahubiri ya Kikristo, wahubiri hutumia usemi wao kimamlaka kukashifu uovu, kuhimiza na kupongeza uadilifu na hata kuamrisha matendo fulani yatekelezwe na waumini.

Asilimia 77 (J=37) ya wasailiwa walieleza kuwa waliteua lugha moja dhidi ya lugha nyingine walipokusudia kutimiza malengo fulani ya kimawasiliano walipokuwa wanahubiri. Wasailiwa walifafanua kuwa amri fulani zilitolewa kwa mamlaka lugha fulani ilipotumiwa ikilinganishwa na nyingine. Kwa upande mwingine, waumini walihimizika kwa njia bora zaidi iwapo lugha fulani ingetumiwa. Hali hii inaonyesha wazi kuwa halikuwa jambo rahisi kwa mhubiri kutumia lugha moja pekee kuanzia mwanzo hadi mwisho wa mahubiri yake. Lugha ilichanganywa ili kutimiza malengo fulani ya kimawasiliano. Uteuzi wa lugha zilizo changanywa katika mahubiri ya Kikristo jijini Nairobi ulifanywa kama mkakati wa kimawasiliano uliolenga kutimiza malengo anuwai ya kimawasiliano. Tunaweza kuhitimisha hoja zilizojadiliwa katika sehemu iliyotangulia ambazo ziliathiri uchaguzi wa lugha iliyotumiwa katika mahubiri ya Kikristo jijini Nairobi kupitia kwa jedwali lifuatalo:

Hoja zinazoathiri Uteuzi wa Lugha

Hoja	Athari
Washirika	Umilisi wa lugha, lugha inayopendelewa, hadhi ya kijamii na kiuchumi, umri wa mzungumzaji, jinsia, kazi, kiwango cha elimu, uhusiano uliopo baina ya wazungumzaji, nguvu/uwezo na mielekeo kuhusu lugha.
Muktadha	Mahali au mandhari ya mawasiliano, kiwango cha urasmi wa mazungumzo, kiwango cha ukaribu au utangamano uliopo baina ya washiriki kwenye mazungumzo.
Yalimo kwenye mazungumzo	Mada ya mazungumzo, aina ya msamiati unaohitajika katika mazungumzo, ujumbe unaowasilishwa.
Uamilifu wa mazungumzo	Kuinua hadhi ya mzungumzaji, kukuza uhusiano wa kijamii, kutenga baadhi ya hadhira, kusihi, kushuritisha au kutoa amri.
Malengo ya mazungumzo	Kusisitiza ujumbe, utambulisho, kuamuru, kuonya, kutawaza au kupongeza.

Asili: Data ya nyanjani

Hitimisho

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti, ni dhahiri kuwa hoja zilizoathiri uteuzi wa lugha katika mahubiri ya Kikristo jijini Nairobi zilikuwa aina ya washiriki katika mazungumzo, muktadha wa mazungumzo, yaliyomo kwenye mazungumzo, uamilifu wa mazungumzo na malengo ya mazungumzo. Wahubiri wa Kikristo jijini Nairobi waliteua lugha ya kutumia katika mahubiri wakizingatia jukumu mahususi ambalo lingetekelezwa na lugha iliyoteuliwa kufanikisha malengo yao ya Kimawasiliano. Wahubiri wa Kikristo jijini Nairobi waliteua lugha wakizingatia aina ya hadhira waliokusudia kuihubiria. Wahubiri walizingatia umilisi wa lugha wa washirika wao, hadhi yao, umri wao, kiwango chao cha elimu na lugha walizozielewa kwa urahisi. Uteuzi wa lugha unaweza kutumiwa kuonyesha mielekeo ya wazungumzaji kuhusu lugha fulani. Wingilugha ni mtaji unaosaidia uteuzi wa lugha kwa ajili ya kutimiza majukumu mbalimbali ya kimawasiliano. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa lugha iliyoeweka miongoni mwa waumini wengi ilikuwa Kiswahili. Hii ndiyo sababu ya kupendelewa kwake katika mahubiri ya Kikristo jijini Nairobi. Muktadha wa mahubiri ulikuwa wa kanisani ambao ulihitaji kiwango cha juu cha urasmi na udumishwaji wa utangamano. Hili liliwafanya wahubiri kuteua Kiswahili kwa vile idadi kubwa ya waumini wao walielewa Kiswahili na vilevile waliibuka kutoka kwenye jamii-lugha mbalimbali nhini.

Utafiti huu ulibainisha kuwa kila lugha iliyotumiwa katika mahubiri ya Kikristo jijini Nairobi ilitekeleza majukumu ya kiisimu, kiisimujamii, kisaikolojia na kitamaduni. Wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili walikuwa na umilisi bora wa

lugha hiyo ikilinganishwa na Kiingereza. Kimsingi, wahubiri walitumia Kiswahili kama lugha ya mawasiliano mapana ya kidini na waumini wao ili kudumisha utangamano, umoja na wiano. Lugha ya Kiswahili ilipendelewa zaidi katika mawasiliano ya kidini kutokana na mielekeo chanya ya wahubiri kuhusu. Isitoshe, lugha ya Kiswahili ilitumiwa na wahubiri kukuza hisia za utamaduni wa kitaifa na wala sio wa kimbari miongoni mwa waumini. Hilo liliwafanya waumini wajione kuwa katika jumuiya moja iliyo na utambulisho wa kidini. Kiingereza kwa upande mwingine, kilitumiwa kwenye mawasiliano na hadhira ya kiusomi. Kiingereza kilitumiwa kudumisha hadhi ya juu na vilevile kwenye mawasiliano yaliyonuiwa kutenga sehemu ya hadhira iliyokosa umilisi wa lugha hiyo.

Marejeleo

- Austin, J. L. (1962). *How to Do Things with Words*. Cambridge: Harvard University Press.
- Bamgbose, A. (1992). *Speaking in Tongues: Implications of Multilingualism for Language Policy in Nigeria*. Ibadan: Wemilse Press
- Blom, J. P. & Gumperz, J. J. (1972). Social Meaning in Linguistic Structures: Code-switching in Norway. In J. J. Gumperz & D. Hymes (eds.). *Directions in Sociolinguistics: The Ethnography of Communication*. New York: Holt, Rinehart, and Winston. Pg. 407-434
- Chimerah, R. (1998). *Kiswahili: Past, Present and Future Horizons*. Nairobi: Nairobi University Press.
- Coulmas, F. (1997). *The Handbook of Sociolinguistics*. Oxford: Blackwell.
- Crystal, D. & Davy, D. (1969). *Investigating English Style*. London: Longman
- Dweik, B. & Qawar, H. (2015). Language Choice and Linguistic Attitudes in a Multilingual Arab Canadian Community: Quebec-Canada: A Sociolinguistic Study. *British Journal of English Linguistics*, Vol. 3 (1): 1-12.
- Fasold, R. (1990). *The Sociolinguistics of Language*. Oxford: Blackwell.
- Fink, T. S. (2005). *Attitudes Towards Languages in Nairobi*. Unpublished Masters of Linguistics Thesis, University of Pittsburg.
- Gal, S. (1979). *Language Shift: Social Determinants of Linguistic Change in Bilingual Austria*. New York: Academic Press.
- Gumperz, J. J. (1964). Linguistic and Social Interaction in two Communities. *American Anthropologist*, Vol. 66 (6): 137-153.
- Hymes, D (1964). *Language in Culture and Society*. New York: Harper and Row.
- Kendal, M. B. (1980). Radical Grammars: Interplay of Form and Function. In Giles, H. (ed) *Language: Social Psychological Perspective*. London: Basil & Blackwell. Pg. 329-334.
- KNBS (2020). *The 2019 Kenya Population and Housing Census: Counting Our People for the Implementation of Vision 2030*. Nairobi: KNBS.
- Kouega, J. P. (2008). Language, Religion and Cosmopolitanism: Language Use in the Catholic Church in Yaoundé, Cameroon. In *International Journal of Multilingualism*, Vol 5 (2): 140–153.
- Maya, D. K. (2006). Language policies- impact on language maintenance and teaching: Focus on Malaysia, Singapore, Brunei and the Philippines. *The Linguistics Journal*, Vol. 1: 155-191.

- Moshi, L. (2006). The Globalized World Languages: The Case of Kiswahili. In Olaoba, F. A. and Pemberton, M. (eds) *Selected Proceedings of the 36th Annual Conference on African Linguistics*. Somerville, MA: Cascadilla Proceeding Project. Pg. 166-175
- Myers-Scotton, C. (1983). The Negotiation of Identities in Conversation: A Theory of Markedness and Code Choice. *International Journal of the Sociology of Language*, Vol. 44: 115-136.
- Omoniyi, T. (2012). Multilingualism and Religion. In A. Creese, A. Blackledge and M. Martin-Jones (eds.) *The Routledge Handbook of Multilingualism*. New York: Routledge.
- Parkin, W. (1974). Language Use in Kenya. In Whiteley, W. (ed) *Language in Kenya*. Nairobi: Oxford University Press. Pg. 134-165
- Platt, J. (1980). The Relation Between Accommodation and Code-Switching in a Multilingual Society. In Giles (ed) *Language: Social Psychological Perspective*. London: Basil & Blackwell. Pg. 178-192.
- Schiffrin, D. (1994). *Approaches to Discourse*. Oxford: Blackwell.
- Searle, J. R. (1969). *Speech Acts: An Essay in the Philosophy of Language*. Cambridge University Press.
- Ugot, M. (2009). Language Choice, Code-switching and Code-mixing in Biase. *Global Journal of Humanities*, Vol. 8 (2): 27-35
- Wangia, J. I. (1992). *Language Choice and Use by Lower Primary School Children in a Multilingual Urban Setting: Nairobi*. Unpublished M.A. Thesis, Kenyatta University, Nairobi.
- Yakub, A., Matu, P. M. & Ongarora, D. O. (2012). Language Use and Choice: A Case Study of Kinubi in Kibra, Kenya. *International Journal of Humanities and Social Sciences*, Vol. 2. (4): 99-100.